ISSN 0856 - 0323

MWAKA WA 85

TOLEO NA. 44

29 Oktoba, 2004

GAZETI

BEI SH. 200/= LA DAR ES SALAAM

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

—0—

Limetolewa kwa Idhini ya Serikali na Kuandikishwa Posta kama Gazeti

YALIYOMO

	Taarifa ya Kawaida	Uk.
Kuajiriwa na kukabidhiwa Madaraka	Na. 675	471
Notice *re* Supplement	Na. 676	472
Tanzia		472
Kupotea kwa Hati za Kumiliki Ardhi...	Na. 677-82	472/3
Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati za Kugawa Ardhi	Na. 683	473
Uchunguzi wa Mgogoro wa Kikazi	Na. 684	474
Uthibitisho wa Usimamizi wa Mirathi	Na. 685-6	477/8

KUAJIRIWA NA KUKABIDHI MADARAKA

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 675

Ofisi ya Rais–Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Kuwa Afisa Tawala Daraja la III:–

BW. DONALD BOMBO, kuanzia tarehe 9/5/2002.
BW. MAGOHU Z. CHAMRIHO, kuanzia tarehe 27/5/2002.
BW. NESTORY PATRICK, kuanzia tarehe 27/5/2002.
BI. DOROTHY D. NDABI, kuanzia tarehe 1/5/2002.
BW. JAMES I. SIULANGA, kuanzia tarehe 15/5/2002.
BIBI GLORIA O. MWASAMAJA, kuanzia tarehe 22/5/2002.
BW. LAWRENCE L. SAWE, kuanzia tarehe 16/5/2002.
BW. LAZARO A. KISUMBE, kuanzia tarehe 16/5/2002.
BI. AISHA H. MPONEZYA, kuanzia tarehe 13/5/2002.
BW. JOSEPH N. MFANGAVO, kuanzia tarehe 23/5/2002.
BW. JAMES J. KIBAMBA, kuanzia tarehe 6/6/2002.
BW. WILFRED MYUYU, kuanzia tarehe 1/6/2002.
BW. DAUDI I. HUNGU, kuanzia tarehe 1/8/2001.
BW. OPTATUS H. FIDELIS, kuanzia tarehe 3/8/2001.

Kuwa Afisa Tawala Daraja la II:–

BW. BONIPHACE M. CHAMBI, kuanzia tarehe 15/9/2003.
BW. CHARLES S. IKOLO, kuanzia tarehe 15/9/2003.
BI. SUBILAGA MWANDIGA, kuanzia tarehe 16/9/2003.
BIBI ATHANASIA P. KABUYANJA, kuanzia tarehe 8/9/2003.
BI. ELIAINENYI M. MARIKI, kuanzia tarehe 12/92003.
BI. FLORA WILLIAM, kuanzia tarehe 12/9/2003.
BI. JANET S. MISHINGA, kuanzia tarehe 26/9/2003.
BW. FILOTHEUS S. MANULA, kuanzia tarehe 15/9/2003.
BI. EDWARD M. WAMBURA, kuanzia tarehe 2/9/2003.
BW. ELIUS NYAKIA, kuanzia tarehe 30/9/2003.
BW. FRANCIS N. TUMBO, kuanzia tarehe 26/9/2003.
BI. BEATRICE M. ALEXANDER, kuanzia tarehe 11/9/2003.
BW. LAZARO WILSON MWANKENJA, kuanzia tarehe 1/10/2003.
BW. BERNARD D. URASSA, kuanzia tarehe 8/9/2003.
BW. NESTORY C. MUJUNANGOMA, kuanzia tarehe 18/9/2003.
BW. ABBAS J. KAYANDA, kuanzia tarehe 1/9/2003.
BW. ZACHARIA A. DIDA, kuanzia tarehe 1/10/2003.
BW. YOHANA M. KASITILA, kuanzia tarehe 6/10/2003.
BW. GASTO K. GASPER, kuanzia tarehe 11/9/2003.
BW. CELINA M. MAONGEZI, kuanzia tarehe 12/9/2003.
BW. ABDON D. MALLYA, kuanzia tarehe 1/9/2003.
BW. SOSTHENES J. MAYOKA, kuanzia tarehe 1/10/2003.
BI. VEDASTINA K. JUSTINIAN, kuanzia tarehe 1/9/2003.

Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka:–
(inaendelea tazama uk. wa 478)

Matangazo yahusuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma yaweza kuchapishwa katika Gazeti. Yapelekwe kwa **Mhariri, Idara Kuu ya Utumishi-Ofisi ya Rais, S. L. P. 2483, Dar es Salaam, Simu za Ofisi 2118531/4.** Kabla ya *Jumamosi ya kila juma.*

Limepigwa Chapa na Mpigachapa Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam - Tanzania

TANZIA

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha Ndugu Venance Meli Baikye - Aliyekuwa Afisa Muuguzi Daraja la II, Mtumishi wa Hospitali ya Mkoa Kagera, kilichotokea tarehe 17/9/2004 katika hospitali ya Mkoa wa Kagera.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 676

Notice is hereby given that an Instrument, Sheria Ndogo, By-laws and Orders as set out below, have been issued and are published in subsidiary Legislation Supplement No. 44 dated 29th October, 2004 to this number of the *Gazette*:–

The Bukombe District Council (Health Service Board Establishment) Instrument, 2004 (Government Notice No. 451 of 2004).

Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe (Ada na Ushuru) mwaka 2004 (Tangazo la Serikali Na. 452 la mwaka 2004).

Sheria Ndogo za (Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, 2004 (Tangazo la Serikali Na. 453 la mwaka 2004).

Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu (Uchangiaji katika Ujenzi wa Shule za Sekondari) za mwaka 2004 (Tangazo la Serikali Na. 454 la mwaka 2004).

Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Magu (Ada na Ushuru) za 2004 (Tangazo la Serikali Na. 455 la mwaka 2004).

Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Magu za (Kodi ya Huduma) za 2004 (Tangazo la Serikali Na. 456 la mwaka 2004).

Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, 2004 (Tangazo la Serikali Na. 457 la mwaka 2004).

Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, 2004 (Tangazo la Serikali Na. 458 la mwaka 2004).

The Bukombe District Council (Community Health Fund) By-laws, 2004 (Government Notice No. 459 of 2004).

Order under the Water Works Ordinance (Government Notice No 460 of 2004).

Order under the Community Service Act, 2002 (Government Notice No. 461 of 2004).

Order under the Corporation Sole Establishment Act, 1974 (Government Notice No. 462 of 2004).

Order under the Public Corporation Act 1992 (Government Notice No. 463 of 2004).

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 677

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Namba: 378-DLR.
Mmiliki aliyeandikishwa: AGUSTINO MKALIMOTO WA S. L. P. 247, IRINGA.
Mwombaji: The Consolidated Holding Corporation wa S. L. P. 21195, Dar es Salaam.
Ardhi: LO. No. 45715, Kiwanja Na. 137, Kitalu X Iringa Municipality.
Eneo: FUTI ZA MRABA 3890.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana irudishwe kwa Msajili wa Hati Msaidizi Mwandamizi Mkuu, S. L. P. 2984, Mbeya.

7 Oktoba, 2004

S. T. KESSY,
Msajili wa Hati Msaidizi
Mwandamizi Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 678

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Namba: 186166/75.
Mmiliki aliyeandikishwa: PASCHAL NERE MATUNDA.
Ardhi: Kiwanja Na. 111 Upanga, Jijini, Dar es Salaam.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana irudishwe kwa Msajili wa Hati S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
25 Oktoba, 2004

REHEMA NTIMIZI,
Msajili wa Hati Msaidizi
Mwandamizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 679

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Namba: 21001.
Mmiliki aliyeandikishwa: HAWA ABDALLAH.
Ardhi: Kiwanja Na. 644 Kitalu 'C' Sinza, Jijini Dar es Salaam.
Mwombaji: Abdallah Hassan Namwete.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana irudishwe kwa msajili wa Hati, S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
20 Oktoba, 2004

REHEMA NTIMIZI,
Msajili wa Hati Msaidizi
Mwandamizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 680

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Namba: 26995.
Mmiliki aliyeandikishwa: EUGEN BAMARWENDA.
Ardhi: Kiwanja Na. 42 Kitalu 'B' Mikocheni High Density, Jijini Dar es Salaam.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
13 Juni, 2004

REHEMA NTIMIZI,
Msajili wa Hati Msaidizi
Mwandamizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 681

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Namba: 10766.
Mmiliki aliyeandikishwa: KILOSA CO-OPERATIVE UNION LIMITED.
Ardhi: Kiwanja Na. 6 Kitalu 'K' Kilosa Mjini.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
28 Septemba, 2004

REHEMA NTIMIZI,
Msajili wa Hati Msaidizi
Mwandamizi Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 682

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi
(Sura 334)

Hati Namba: 18906.
Mmiliki aliyeandikishwa: AMIRALI JAFFER KHAKOO.
Ardhi: Kiwanja Na. 13 Kitalu 'A' Main Street Kilosa Township.
Mwombaji: Kilosa Co-operative Union (1985) Limited.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana irudishwe kwa Msajili wa Hati, S. L. P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
28 Septemba, 2004

REHEMA NTIMIZI,
Msajili wa Hati Msaidizi
Mwandamizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 683

WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI
Sheria ya Ardhi ya 1999
(NA. 4 YA 1999)

UTEUZI WA WAJUMBE WA KAMATI ZA KUGAWA ARDHI
Chini ya fungu la 12

Kutokana na uwezo niliopewa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, 1999 ninawateua wafuatao kuwa wajumbe wa Kamati za Kugawa Ardhi kama zilivyoundwa katika Kanuni–The Land (Allocation Committee) Regulations, 2001, G. N. No. 72 of 4th May, 2001:–

A. Maafisa wafuatao kutokana na nyadhifa zao katika Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, Dodoma:

1. Mkurugenzi Mkuu	–	Mwenyekiti
2. Mkurugenzi wa Miliki	–	Katibu
3. Afisa Mteule	–	Mjumbe
4. Mkurugenzi wa Mipango	–	Mjumbe

B. Maafisa waajiriwa wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Waheshimiwa Madiwani wafuatao:–

Serial No.	*Majina ya Wajumbe*	*Cheo/Jinsia*
1.	G. Y. Chetty	Meya wa Manispaa (Me)
2.	J. K. Mambo	Diwani (Me)
3.	M. A. Sadiki	Diwani (Ke)
4.	W. E. Kijoti	Mkurugenzi wa Kusimamia Mazingira (C. D. A.)
5.	A. K. O. Mbwambo	Mkurugenzi wa Uhandisi na Ujenzi (C. D. A.)
6.	Monica P. Z. Kwiluhya	Mkurugenzi wa Manispaa
7.	C. M. Kazi	Mkurugenzi wa Bunge na Siasa (Ofisi ya Waziri Mkuu)
8.	J. Rogati	Mpima Ardhi (Sekretarieti ya Mkoa)
9.	A. S. Kilingo	Katibu wa Shirika (C. D. A.)
10.	A. Salingwa	Afisa Ardhi (Manispaa)
11.	L. G. Mtenga	Meneja wa Mradi LCH, CDA

Dar es Salaam
18 Oktoba, 2004

GIDEON ASIMULIKE CHEYO (MB.),
Waziri wa Ardhi na
Maendeleo ya Makazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 684

UCHUNGUZI WA MGOGORO WA KIKAZI NA. 11 WA 1999

baina ya

OTTU/TUICO KNY. A. S. KAZUBA

na

N. B. C. HOLDING CORP.

UAMUZI

Mlalamikaji Bw. Abubakar Sanzu akiwa Chief Manager wa NBC Lindi alipokea mnamo tarehe 8/1/96 barua ya kuachishwa kazi kuanzia tarehe 18/12/1995 yenye Kumb. BTB/JB/Vol.II/1788 iliyotolewa kama Kielelezo P. 2 kama adhabu ya makosa yakinidhamu ambayo Bodi ya Wakurugenzi ya NBC ilimtia hatiani kwenye kikao chake cha 265 kwa kukiuka aya za 3(e), 6(a) na 4 (e) ya Kanuni za Nidhamu za NBC (NBC Revised Code of Conduct). Kielelezo hicho kilimjulisha kuwa ingawaje alipaswa afukuzwe kazi kadri kima cha adhabu cha juu cha kosa hilo kilivyo, wao walimpunguzia adhabu na kumwachisha kazi tu pamoja na kumlipa marupurupu yake yote ya kuachishwa kazi ambayo ni mshahara wa mwezi mmoja badala ya notisi, malipo ya likizo kwa siku 56, usafirishwaji wake na mizigo hadi kwao alikotokea (place of Domicile) na michango yake ya akiba ya uzeeni.

Mlalamikaji hakuridhika na kutiwa hatiani kwa makosa ya nidhamu aliyoshtakiwa nayo na kwa adhabu aliyopewa. Kwa hiyo aliishtaki NBC inaelekea kwa OTTU/TUICO wilayani Lindi kufuatana na ushahidi wa kiapo (kama PW. 1) wa mlalamikaji kwamba ndivyo alivyoanzisha mgogoro huu wa uchunguzi. OTTU/TUICO Wilaya ya Lindi, ndio ameeleza waliompelekea mgogoro huu kwa Katibu Mkuu wa OTTU Bw. B. Mpangala ambaye yeye kwa mara ya kwanza ndiye (Bw. B. Mpangala, Katibu Mkuu wa OTTU) aliyemwandikia Kamishna wa Kazi (TUC/TD/ENQ/1/2/2 ya tarehe 2/2/96 akimwomba Kamishna atumie kifungu cha 8 cha Sheria ya Kazi kuchunguza mgogoro huu. Yeye mwenyewe Katibu Mkuu wa OTTU hakueleza kwenye barua hiyo au mahali popote pale kwamba mgogoro huu ulifikafikaje kwake. Ila nakala ya barua yake aliinakilisha kwa Katibu wa Mkoa TUICO Mkoa wa Lindi na kwa mlalamikaji Bw. A. S. Kazuba c/o NBC Lindi bila kutaja kumbukumbu zao hao akina Katibu wa Mkoa wa TUICO Mkoa wa Lindi na Bw. A. S. Kazuba c/o NBC Lindi. Kwa taratibu za kiofisi kwa vile hakunukuu kumbukumbu za barua za hao watu wawili wa Lindi – Katibu wa Mkoa na Bw. A. S. Kazuba kuna uwezekano kuwa malalamiko ya mgogoro huu hayakufanyika kwake Katibu Mkuu wa OTTU kutokea kwao au kama ndio waliompelekea malalamiko haya basi yeye Katibu Mkuu hakutaka kuonyesha hivyo alipopelekea shauri hili kwa Kamishna wa Kazi. Sasa tatizo hili limetatuliwa kwani PW. 1 ameeleza kuwa ni OTTU Lindi waliopeleka mgogoro huu kwa katibu mkuu OTTU, Dar es Salaam. Kwa vyovyote vile mgogoro huu haukupitia kabisa katika ngazi ya Afisa Kazi wa Wilaya au Mkoa wa Lindi na hakuna hati ya Afisa Kazi yeyote kuonyesha kuwa huyu mlalamikaji alikuwa kwenye uongozi wa mwajiri chini ya Kifungu cha 10 cha Sheria ya Mahakama ya Kazi. Tokea Kamishna wa Kazi apelekewe mnamo tarehe 2/2/96 mgogoro huu na Katibu Mkuu wa OTTU mapema mara tu baada ya mlalamikaji kupokea barua ya kuachishwa kazi mnamo tarehe 8/1/96 yeye Kamishna wa Kazi amekaa na mgogoro huu kwa zaidi ya miaka 3 hadi tarehe 25/3/99 ndipo alipoufikisha mgogoro huu kwenye mahakama hii kwa barua yake yenye Kumb. Na. KZ/U.10/773/10 ya tarehe 24/3/99. Mbele yake Kamishna wa Kazi majibishano yao yote kati ya mwajiri na mlalamikaji yalikuwa yamekamilika hadi kufikia tarehe 26/6/97. Jalada lake Kamishna wa Kazi limekaa kwake tokea hapo bila kushughulikiwa hadi hapo waliposukumwa na TUICO mnamo tarehe 13/1/99 kwa barua yao TUC/TD/ENQ/1/2/9 ndipo sasa Kamishna wa Kazi alileta mgogoro huu mnamo hiyo tarehe 24/3/99 kwa barua yake KZ/U.10/MG/773/10. Hapa Mahakama ya Kazi napo tokea mgogoro huu umefunguliwa na Kamishna wa Kazi wahusika wamejibizana na hadi mgogoro umesikilizwa imechukua mwaka 1 na miezi 9 hadi leo uamuzi unatolewa.

Miongoni mwa maombi ya mlalamikaji ni kupewa na Mahakama hii haki ya kurudishwa kazini na kulipwa "haki zake zote za ajira yaani mishahara yake na marupurupu yake yote tangu tarehe alipofukuzwa kazi hadi sasa" (In inverted commas) nimenukuu kutoka kwenye kumbukumbu za madai ya Mlalamikaji aya ya 7(c).) Jee, kama mlalamikaji atashinda kwenye mgororo huu Mwajiri awajibishwe kulipa mishahara na marupurupu ya mfanyakazi huyu hata kama yalifanyika makosa ya kumwachisha kazi isivyostahili kwa uzembe au uvivu na matatizo ya kutomaliza mgogoro huu ya ofisi za Kamishna wa Kazi na Mahakama hii kwa takribani sasa miaka 4 mizima tokea tarehe 2/2/96 Kamishna wa Kazi alipopelekewa mgogoro huu hadi leo tarehe 19/12/2000 ambapo sasa ndipo uamuzi huu unatolewa?

Na hata sasa tushukuru kupitishwa kwa sheria Na. 2/2000 iliyoanza kutumika tarehe 14/4/2000 ambayo sasa imeruhusu kuendelea kusikilizwa kwa mgogoro iwapo Waungwana Washauri wa Mahakama watapata matatizo ya kutokuweza kuhudhuria na kuendelea na kikao cha mahakama kwani tulianza, kwenye mgogoro huu na washauri wa Mahakama wawili kwenye kikao cha Sessions cha kanda kule Mbeya mnamo tarehe 14/8/2000 ambao ni Mwungwana Bw. Mahenge (ATE) na Mwungwana Mama Kabigi (OTTU) hadi upande wa mlalamikaji ukafunga kesi yake baada ya PW. 1 A. S. Kazuba mwenyewe kutoa ushahidi na utetezi ulianza na ukachukuliwa ushahidi wa DW. 1 Charles Douglas Lukaya. Baada ya hapo utetezi uliomba muda zaidi wa kuita mashahidi wengine na tuliahirisha hadi hapa Dar es Salaam ambapo kwenye kikao cha hapa Dar es Salaam wale waungwana Wazee wa Mahakama wa Mbeya hawakuweza kupata nafasi ya kuja toka Mbeya ili kuendelea kumalizia kusikiliza mgogoro huu. Kwa hiyo tuliendelea bila Waungwana Washauri wa Mahakama hapa mnamo tarehe 20/10/2000 chini ya Sheria hiyo mpya Na. 2/2000 tulipochukua ushahidi wa DW. 2 Monas Wilson Parsalaw na utetezi ukafunga kesi yake kwa upande wa utetezi. Muhtasari wa kila upande wa mwisho umemalizika kuletwa mahakamani kwa maandishi mnamo tarehe 20/11/2000. Kwa hiyo basi uamuzi huu unatolewa bila faida ya maoni ya Waungwana Washauri wa Mahakama. Mlalamikaji Bw. A. S. Kazuba amewakilishwa wakati wote na Bw. Peres Jonathan kutoka TUICO Makao Makuu Dar es Salaam na mlalamikiwa NBC Holding Corporation amewakilishwa mwanzoni na Msomi Bw. Nyabiri, Wakili toka Dodoma na baadaye aliendelea kumalizia utetezi kuanzia kwenye ngazi ya DW. 2 Msomi Bw. Rweyongeza Wakili kutoka huko huko Dodoma baada ya Msomi Bw. Nyabiri kuungua na kufanyiwa operation.

Hadidu za maamuzi ya mgogoro huu zilitengenezwa mwanzoni mwa kuanza kusikiliza mgogoro huu kama ifuatavyo:–

1. Jee mlalamikaji alifanya makosa yoyote yale ya kinidhamu yaliyopelekea kuachishwa kazi?

2. Jee mlalamikaji alipewa fursa ya kujitetea kabla ya kuadhibiwa kwa kuachishwa kazi?

3. Jee Kanuni za benki zilizotumika kumwadhibu mlalamikaji ndizo zilizopaswa zitumike?

4. Jee kuachishwa kazi kwa mlalamikaji kulikuwa halali?

5. Jee kila upande una haki gani za kupewa na mahakama hii? Wakati mgogoro unaanza kusikilizwa mlalamikaji alikubali kuondoa hoja ya tukio la kufukuzwa kazi na badala yake alikubaliana na Mwajiri kuwa alichofanyiwa ni kuachishwa kazi tu, na sio kufukuzwa kazi. Kwa hiyo, kwa kukubaliana kwa pande zote mbili hoja ilipitishwa na mahakama kwamba mlalamikaji aliachishwa kazi na sio kufukuzwa kazi.

Nitaanza kuamua hadidu ya kwanza ambayo inahoji kama mlalamikaji alifanya makosa ya kwanza ambayo inahoji kama mlalamikaji alifanya makosa yoyote yale ya kinidhamu yaliyopelekea aachishwe kazi. Makosa yenyewe ya nidhamu yanayodaiwa kuwa aliyafanya mlalamikaji yamo kwenye Kielelezo P. 1 alichokitoa Mahakamani kama ushahidi wake mlalamikaji mwenyewe na yana vipengele vinne ambavyo ni kuidhinisha malipo kwenye cheki za nje ambazo hazina hela (uncleared upcountry cheques) bila kupata uthibitisho wa awali kutoka kwenye tawi husika kuwa anazo hela (without obtaining pre-clearance) kinyume cha aya ya 3(e) ya Kanuni za Benki zilizorekebishwa na utendaji kazi. "Hizo uncleared up-country cheques" husika ni za Pirbaksh Abdulasamad Mulla Na. J02941032 ya tarehe 29/6/93 ya Shs. 5 milioni/- iliyorudishwa bila kulipwa mnamo tarehe 14/8/93 na Cheque No. J 02935820 ya Shs. 1,350,000/- iliyorudishwa bila kulipwa mnamo tarehe 1/11/1993 pamoja na madei yake mengineyo ya huyo Pirabaksh Abdulasamad Mulla ya Shs. 9,301,679/30 na Shs. 7,500,000/- inayoleta jumla ya fedha zilizokopeshwa kufikia Shs. 13,850,000/-.

Kwa upande wa Bw. Arifs yeye alidaiwa kuidhinishwa na mlalamikaji kati ya tarehe 5/4/93 na tarehe 30/6/93 jumla ya fedha zilizozidishwa (overdraw) kwa kiasi cha Shs. 19,450,000/-.

Kosa la pili alilodaiwa mlalamikaji alilitenda kinidhamu ni la kushindwa kwa hiari na kwa makusudi kukusanya ushuru wa ada za Benki (NBC Revenue) kwa njia ya riba kinyume cha aya 6 (a) ya Kanuni za utendaji kazi za Benki (NBC code of conduct). Maelezo ya kosa hili ni kwamba mlalamikaji alitoa mikopo ya juu ya zaidi kuliko fedha zilizopo benki (overdraft) kwa kiasi cha shs. 13,000,000/- kwa Pirbakash A. Mulla, Shs. 8,100,000/- kwa Arifs, Shs. 20,000,000/- kwa BP Highlands Services station Shs. 230 milioni kwa Trans Auto Express na Shs. 114 milioni/- kwa Southern Highlands Estates Ltd- Jumla Shs. 385,100,000/- ambapo Birbaksh A. Mulla na Arifs walihusika na Shs. 21m/- alizozidishwa kukopesha kwao.

Kosa la tatu lilihusu kushindwa kufanya kazi za Meneja Tawi la NBC na hivyo kuhatarisha fedha za benki kinyume na Aya ya 4 (e) ya Kanuni za Benki zilizorekebishwa. Maelezo ya shtaka hili ni yale yale kama ya shtaka la kwanza na la pili.

Shitaka la nne ni la kutenda kazi kwa namna mbaya ya kutoendeleza maslahi ya Benki, jina zuri la Benki na mafanikio ya Benki kinyume na aya ya 1 (t) ya Kanuni za Benki.

Mbele ya Mahakama hii kwa njia ya ushahidi wake na kiapo na kwa njia ya vielelezo P.1 – P.5 alivyotoa kwenye ushahidi wake mlalamikaji kama PW. 1 Abubakar Sanzu Kazuba amepinga mashtaka hayo kuwa si ya kweli, kwani alihamishiwa Lindi tawi la NBC mnamo tarehe 30/6/93 kutoka tawi la NBC Mshindo Iringa ambako ndiko makosa hayo yamedaiwa kutendeka. Baada ya zaidi ya miaka miwili kupitia ndipo, akiwa Lindi, alipoletewa mashtaka hayo kwenye Kielelezo P.1. Bw. Jonathan mwakilishi wake mlalamikaji amefafanua utetezi huu kwamba kuna cheque nyingi ambazo ziliidhinishwa hata baada ya yeye mlalamikaji kuhamia Lindi baada ya tarehe 30/6/93 ambazo hazimhusu kwenye ushahidi wake wa kiapo yeye mwenyewe mlalamikaji kama PW. 1 ameeleza kuwa ni kweli ziliidhinisha "Country Cheque on uncleared effects" kwani alikuwa na madaraka ya kufanya hivyo chini ya Kanuni za Benki alizotoa kama Kielelezo P. 3 ili mradi aidhinishe 75% ya kiasi kilichoko kwenye "Country Cheque" hiyo na kiasi cha 25% tu cha "Country Cheque" hiyo ndicho anatakiwa aidhinishe "Country Cheque" ikisharudishwa toka "NBC tawini kwake kwenye account hiyo. Nanukuu baadhi ya maneno yake mwenyewe PW.1 ya kiapo kama ifuatavyo:– Nanukuu "manuscript" ya ushahidi wake toka kwenye jalada la Mahakama"–

> "Tuhuma kwamba niliidhinisha cheques za Shs. 19,450,000/- bila kuidhinishwa kwamba fedha hizo ziko kwenye matawi zilikotoka "cheques" hizo ni sawa. Utaratibu ni kwamba mteja akiweka hundi ya nje kwenye account yake Meneja alikuwa anaweza kuidhinisha 75% ya kiasi cha fedha ya hundi hiyo papo kwa papo na asilimia 25% iliyobaki iliidhinisha baada ya Benki ya Tawi lake kuidhinisha; fedha hizo. Kutokana na maagizo hayo yamo kwenye waraka Na. 60/91 wa tarehe 6/7/91. Meneja alikuwa na madaraka ya kuidhinisha utoaji wa fedha za hundi ili mradi atekeleze na awe na sifa za kwenye waraka huo. Hakulazimika tena kupata uthibitisho wa country cheque hizo kutoka kwenye tawi lake zilikotoka country cheque hizo. Naomba kutoa waraka huo kama kielelezo."

Mah: Napokea Waraka wa tarehe 6/7/91 Ref. NBC/DIA/D.10/10 kama Kielelezo P. 3.

(Shahidi anasoma mamlaka ya kuidhinisha hundi bila kupata idhini ya Tawi ambako cheque imetoka. P. 3 aya ya 4 toka juu). Cheque hizi zenye thamani ya Shs. 19,450,000/- mimi niliidhinisha chini ya Kifungu hiki. Mimi sikuhusika na cheque hizi zote. Mimi sihusiki na hundi Shs. 1,350,000/- ya tarehe 30/9/93 kwani mimi nilikuwa nimekwisha ondoka. Kwa hiyo hundi mimi nilikuwa nimekwisha hama kwenda Lindi. Kwa hiyo sikuidhinisha mimi. Hundi zilizobaki niliidhinisha nikiwa hapa Iringa chini ya kifungu hicho. Hakuna hundi nyingine zilizoidhinishwa mimi nikiwa sipo.

Tuhuma ya riba mimi sikuhusika na ukusanyaji wake kwani riba ilikuwa inalipwa baada ya hundi kurudi kutoka kwenye tawi lake la country cheque. Tarehe 5/7/93 nilikuwa nimekwishahamishwa toka Iringa kwenda Lindi. Kwa hiyo nisingeweza kudai riba hiyo.

To Court:

PW. 1 Riba ya 31% inachajiwa baada ya hundi ku"bounce". Kwa hiyo hata kama zile Shs. alizopewa kabla ya kupata clearance zitakuwa hazijalipwa, kwa vile anachukuliwa kuwa ni mkopaji wa kawaida..."

Utetezi wa mlalamikaji Bw. Abubakar Sanzu Kazuba kwamba aliruhusiwa na Waraka Na. 60/91 wa tarehe 6/7/91 kutoa idhini ya kulipwa 75% ya kiasi cha fedha za kwenye Country Cheque papo hapo na 25% inayobaki baada ya cheque hiyo kurudishwa toka tawi lake la Country cheque hiyo limepingwa vikali na shahidi wa mlalamikiwa DW. 1 Charles Douglas Lukuya - Zonal Auditing Director wa NBC wa Mkoa wa Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa aliyekuwa anakaa Iringa wakati wa matukio haya. Ametoa ushahidi kuwa Meneja anayeidhinisha Country Cheque moja kwa moja bila kusubiri clearance ya ilikotoka Country Cheque hiyo lazima ajitahadharishe kuhusu Country cheque hiyo kama ifuatavyo: nanukuu toka kwenye ushahidi wake wa kiapo mahakamani:-

"Kama meneja ameingiza kwenye account ya mteja basi meneja lazima awe na hakika kuwa mteja huyo atakuwa na fedha kwenye tawi lake na kwamba malipo hayo ni genuine transaction. Lazima iwe ni watu wawili wanaofanyiana biashara na huwa wakilipana bila matatizo. Lazima iwe ni account nzuri yenye fedha wakati wote na inaaminika."

Ushahidi huu naridhika, unaweka kima cha discretion ya Meneja mwenye madaraka ya kuidhinisha Country cheque kulipwa papo hapo bila kusubiri clearance ya tawini ilikotoka Country cheque hiyo kuwa ni lazima awe amejiridhisha kuwa fedha hizo zitakuwepo kutokana na tabia ya account zake mwenye cheque hizo kwamba ni kuaminika. Shahidi huyu ametoa ushahidi kuwa cheque zote za P. Mulla zinazohusika na mashtaka haya zilirudishwa bila kulipwa. Nazo ni cheque za tarehe 29/6/93 ya Shs. 5,000,000/-, na cheque ya tarehe 5/7/93 ya Shs. 7,500,000/- toka tawi la Mbarari NBC - Rujewa. Nyingine ya tarehe 30/9/93 ya Shs. 1,350,000/- shahidi huyu alisema haikumhusu mlalamikaji bali Mrs. Mmari aliyembadili kwani mlalamikaji alishahamia Lindi.

Shahidi huyo alitoa Ripoti ya ukaguzi audit report Kielelezo D. 2 kama kinachoonyesha wazi juu ya maidhinisho aliyoyafanya mlalamikaji kwenye Country Cheques hizo.

Shahidi huyu pia alithibitisha kiushahidi kuwa mlalamikaji aliidhinisha malipo ya shs. 2,800,000/- tarehe 5/4/93 kuwa Arifs na Shs. 2,800,000/- mnamo tarehe 21/4/93 kwa huyo huyo Arifs na zote zilirudi bila kulipwa mnamo tarehe 5/7/93. Overdrawn amount ya Arifs amesema ilifikia Shs. 7,861,103/10 bila kuwa na fedha benki kwenye tawi la NBC Mbarali ambako hundi hizo zilitoka.

Shahidi huyu ametoa ushahidi kuwa wote P. Mulla na Arifs ni Wabrushi wa familia moja na ni ndugu na walimvunga mlalamikaji akiuke utaratibu wa Benki kujipatia fedha hizo kama mikopo isiyostahili bila kuwepo biashara yoyote ile waliyokuwa wanalipana kwa-cheque hizo. Alieleza zaidi kuwa madaraka ya Meneja kutoa malipo ya 75% ya Country cheque yaliisha tarehe 26 Machi 1993. Alitoa Waraka Na. 29/93 kama Kielelezo D.1 wa tarehe 26/3/93 uliofuta madaraka ya Meneja kutoa malipo ya Country cheque bila kupata clearance toka tawi la cheque hiyo iliyosema kama ifuatavyo:-

"The Board has decided that all employees of the Bank regardless of their positions identified to have had an element of dishonesty in their execution of duties should be dismissed summarily. An element of dishonesty shall be established in any of the following circumstance:-

1. .....
2. Where an employee without authority pays any cheque against uncleared effect, whether there is loss or not
3. .....
4. Where an employee without authority sanctions overdraft/loans against laid down procedures whether that loan is recovered or not."
5. .....
6. Where an employee does anything without following laid down procedure whether is a loss or not or whether he/she does not act negligently or wilfully.

In all such cases above mentioned no mitigating factors whatsoever are invited ....."

Waraka huu Na.NBC/Ho/C.10/2 Circular No.29/93 ulipelekwa kwa Branch Managers viongozi wote wa Benki nchi nzima pamoja na kwa mlalamikaji. Makosa haya ya mlalamikaji yaliyokuja fanyika Aprili 1993 - Juni 1993 yalimbana mlalamikaji kwani ule uhuru wa kutoa asilimia 75% ya Country Cheque ulikuwa imekomeshwa. Na kwa vyovyote vile mlalamikaji hakuwa anatoa 75% ya fedha za Country Cheques bali alikuwa anatoa fedha zote 100% kama alivyoeleza kiusahihi Msomi Bw. Rweyongeza, Wakili wa mlalamikiwa kwenye final submission yake. Shahidi DW. 1 alifafanua kuwa ingawaje Bw. Kazura alihamishiwa Lindi mnamo tarehe 30/6/1993 lakini aliendelea kuwepo Iringa hadi Agosti, 1993 ndipo alipoondoka Iringa kwenda Lindi na ndiye aliyeidhinisha hata ile hundi ya tarehe 5/7/93. Naridhika na ushahidi wa DW. 1 kuwa ni wa kweli na unaaminika. Utetezi wa mlalamikaji kuwa alifuata Circular ya 91 iliikuwa ni geresha tu ili kufurahisha azma yake ya kuwasaidia akina Mulla na Arifs wajinufaishe na fedha ya NBC isivyostahili na bila kuwa na fedha kwenye tawi lao ya Mbarari Rujewa kinyume na taratibu za Benki. Alibeba jukumu baya na kubwa sana kuwanufaisha wateja wasio waaminifu ambao hawakujali kumuenzi yeye na kumsetiri asiharibikiwe kikazi kwa kulipa kwenye account zao za Mbarali NBC ili cheque hizo zisibounce. Kwa vyovyote vile Circular No. 60/91 Ref. NBC/DIA/D.10/10 ya tarehe 6/7/91 Kielelezo P. 3 ilikuwa mbaya kwa mameneja wa Bank na wateja wabadhilifu kwani iliyowapa mwanya wa kuchota mapesa ya NBC bila Security na bila kulipia Riba mikopo ya Overdrawn accounts au Country cheques. Ni bora haikudumu na ilifutwa miaka 3/4 baadaye na Circular No. 29/93 ya tarehe 26/3/93 Kielelezo D. 2. Hata hivyo overdraft kwa Mulla na Arifs naridhika zilitokea kwa makosa ya kinidhamu ya mlalamikaji.

Nimeridhika kabisa kuwa Bw. A. S. Kazuba mlalamikaji alifanya makosa ya kinidhamu kama alivyoshitakiwa yaliyosababisha hatimaye kuachishwa kazi kwa kujibu hadidu ya kwanza ya uamuzi huu.

Hadidu ya pili ni jee mlalamikaji alipewa fursa ya kujitetea kabla ya kuadhibiwa kwa kuachishwa kazi.

Mlalamikaji ameeleza kuwa baada ya kuhama Iringa bado kuwa aliburutwa tu kwenye mgogoro huu kwani alipewa mashtaka akiwa Lindi na hali vielelezo vya kumsaidia vilikuwa Iringa. Pia amedai kuwa hakushirikishwa kwenye ukaguzi wa mahesabu ya mshataka yanayomhusu. Pia kwenye Bodi aliomba apewe muda wa kupata vielelezo zaidi. Lakini alinyimwa. Na ameeleza kwenye ushahidi wake kwamba kwenye kikao cha Bodi alimwona Mkurugenzi Mtendaji akimnong'oneza Mwenyekiti wa Bodi wakiashiria kumzungumza yeye na kukubaliana labda namna ya kumgandamiza yeye. Pia baada ya kikao Mkurugenzi wa Utumishi Mwendesha mashtaka ya nidhamu alibaki nyuma ndani ya ukumbi wakati yeye akitoka nje akiashiria kuwa mshtaki wake alishiriki kwenye maamuzi ya kumtia hatiani bila yeye kuwepo.

Kwa upande wa mlalamikiwa NBC wameleta ushahidi wa DW. 2 Monas Wilson Parsalaw aliyekuwa Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya NBC. Amejibu tuhuma hizo zote kwa ushahidi wa kiapo kwamba kulikuwa na kesi nyingi kwa hiyo Mkurugenzi wa Utumishi alibakia kwenye Board kuendelea na mashtaka dhidi ya watuhumiwa wengine. Alitoa Kielelezo D. 3 minutes za Board ya tarehe 30/11/95 kwenye kikao cha 265 zinazoonyesha kuwa ni kweli baada ya mlalamikaji kumaliza kesi yake ilianza kesi nyingine ya Mrs. N. A. Mmari ambaye ndiye alimbadili kule Iringa kama Meneja wa Tawi wa NBC Mshindo. Katika kuidhinisha malipo kwa wale wale akina Mulla yeye naye Mrs. Mmari alishtakiwa na kujadiliwa kwenye kikao hicho hicho. Kwa hiyo utawala walipaswa wabaki kihalali ndani ya ukumbi wa kikao ili waendeshe hizo kesi za wafanyakazi wengine. Huyo Mrs. Mmari yeye alifukuzwa kazi kabisa baada ya kutiwa hatiani.

Yakunyimwa haki ya kujitetea au kujieleza ni upuuzi mtupu. Alipewa hati ya Mashtaka na alipewa wiki 2 za kujieleza kwa vyovyote vile alikubali kuidhinisha cheque kwenye unclaimed effects. Wakati wa ukaguzi wa PW. 1 wa tuhuma hizi Meneja aliyekuwepo Iringa ndiye aliyeshirikishwa. Vielelezo alivyotaka avifuate Iringa kama ni vya benki tayari alikwishaelezwa nini ukaguzi wameona na yeye alijulishwa kikamilifu juu ya maelezo ya mashtaka. Hata angekwenda Iringa hangeweza kupata ushahidi zaidi ya ule alioutolea ushahidi wa kiapo hapa mahakamani.

Najibu hoja ya pili kwamba alipewa fursa ya kutosha ya kujitetea kikamilifu. Hakuna haki yoyote aliyonyimwa juu ya yeye kujitetea mbele ya utawala na Bodi ya NBC.

Hoja ya tatu ni jee mlalamikaji alishindwa kukusanya ushuru wa Benki kwenye fedha alizoidhinisha zilipwe kwenye uncleared country cheque au overdraft!

Mlalamikaji amejitetea kuwa riba huwa inaingizwa na inatozwa kwa mteja pale Country Cheque inaporudishwa unpaid baada ya ku-bounce na kurudishwa kwenye tawi lililolipa fedha hizo.

Utetezi huu hauna msingi imara. Kama wateja hawa wangefuata utaratibu wa kukopa fedha benki wangetozwa riba ya 31% kwa wakati huo. Sasa wamejipatia fedha kwa njia ya Country Cheque na overdraft kwa matakwa yake Meneja na kwa kibali na idhini yake bila kutoza ushuru na kwa vyovyote vile riba hiyo haikutozwa kwa wateja hawa wote wa Benki kwa vile walipewa credit facility ambayo ni ya kulipana fedha kibiashara kupitia accounts za Benki na siyo kama mkopo. Kwa kutotumia njia ya kukopa kihalali Benki imekosa riba ambayo ingetozwa kwenye fedha hiyo. Hoja hii inajidhihirisha wazi kuwa riba hiyo haikukatwa. Kwa hiyo anaweza mlalamikaji kubainishwa na kubanwa na hadidu hii barabara kwamba kaikosesha Benki riba ya fedha walizozichota toka Benki.

Hoja ya uhalali wa kutiwa hatiani na, adhabu aliyopewa naridhika ni sawa kwani alitiwa hatiani na alipewa adhabu kihalali.

Hoja ya haki gani wapewe–ninaamua kwamba Yumkini Bw. A. S. Kazula ameshindwa kuyathibitisha malalamiko yake yote kwa hiyo kuachishwa kazi kwake kulikuwa halali na kwa upendeleo au faida yake ukitilia maanani kuwa mwenzie Mrs. Mmari alifukuzwa kabisa kazi wakati yeye alipewa haki kubwa zaidi ya kuachishwa kazi. Kwa hiyo kwenye hadidu hii mahakama hii inaona kuwa mlalamikaji ameshindwa kuthibitisha malalamiko yake.

Mgogoro huu unatupiliwa mbali hivi sasa na kuzaa tuzo hii ambayo nimewasomea mbele ya upande wa mlalamikaji. Msajili atamjulisha mlalamikiwa ambaye hayupo, juu ya tuzo hii.

E. L. K. MWIPOPO, J.,
Mwenyekiti
2/12/2000

Court:

Uamuzi umetolewa mbele ya walalamikaji na bila walalamikiwa kuwepo. Msajili atamjulisha mlalamikiwa juu ya matokeo ya uamuzi huu.

E. I. K. Mwipopo, J.
Mwenyekiti
2/12/2000
Certified true copy of the original.

31/5/2001 B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 685

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Mwanzo Kinondoni, Dar-es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 105 LA MWAKA 2004

Maombi ya Barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Hussein Imamdin, Marehemu
na
Noorbegum Fazal, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu iliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika kuangalia haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 19 mwezi Januari 2005.

Imewasilishwa Jumanne leo tarehe 19 mwezi Oktoba, 2004.

.....
Hakimu wa Wilaya Mkazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 686

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkuu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 102 LA MWAKA 2004

Maombi ya Barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Taherbhai Abbasbhai Aladdin, *Marehemu*

na

Miss Parviz Taherbhai Abbasbhai Alladin, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa wasia kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 25 mwezi wa Januari mwaka wa 2005. Wasia wa Marehemu huyo aliyetajwa umewekwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam 25 mwezi wa Oktoba mwaka 2004.

.....
Hakimu Mkazi Mwandamizi

Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka:– (inaendelea kutoka uk. wa 471)

Ofisi ya Rais–Menejiment ya Utumishi wa Umma

Kuwa Afisa Tawala Daraja la II:–

BW. SAMSON D. MASHALLA, kuanzia tarehe 27/10/2003.
BI. ZIANA T. MLAWA, kuanzia tarehe 13/11/2003.
BI. AGNES D. HUGO, kuanzia tarehe 18/11/2003.
BW. YUSUFU M. KASUKA, kuanzia tarehe 17/9/2003.
BW. JOHN J. NGONYANI, kuanzia tarehe 1/10/2003.
BW. GERVAS I. MUSHI, kuanzia tarehe 22/9/2003.
BW. EGINO G. MAPUNDA, kuanzia tarehe 1/10/2003.
BIBI KHADIJA I. SHAABAN, kuanzia tarehe 1/9/2003.
BW. NURU RINGO, kuanzia tarehe 13/9/2003.
BW. JOHN B. KOMBA, kuanzia tarehe 1/10/2003.
BW. AHMED S. NG'ENI, kuanzia tarehe 16/10/2003.
BW. NDAKI STEPHANO, kuanzia tarehe 11/9/2003.

Kuwa Afisa Utumishi Daraja la II:–

BW. DENIS FABIAN kuanzia tarehe 3/9/2003.
BW. KENNEDY E. MCHOMVU kuanzia tarehe 15/9/2003.
BW. SALUM S. MSANDAGILA kuanzia tarehe 22/9/2003.
BW. CHARLES T. SALYEEM kuanzia tarehe 3/9/2003.
BW. COSMAS S. QAMARA kuanzia tarehe 3/9/2003.
BW. FRANK A. MBILINYI kuanzia tarehe 1/9/2003.
BW. ARNOLD SHADA kuanzia tarehe 1/9/2003.
BI. GLORY BILDARD kuanzia tarehe 17/9/2003.
BI. LEAH J. NDEKUKA kuanzia tarehe 17/9/2003.
BW. ATANAS A. MUTWE kuanzia tarehe 18/9/2003.
BW. BENJAMIN MLIMBILA kuanzia tarehe 17/9/2003.
BI. BERTHA DANFORD RUHONDA kuanzia tarehe 22/1/2004.
BI. SUZANA R. KIWELU kuanzia tarehe 10/9/2003.
BW. SAID MUSSA kuanzia tarehe 9/9/2003.
BW. CHRISTMAS GOWELE kuanzia tarehe 11/9/2003.
BI. ESTERIA G. MRINGO kuanzia tarehe 9/9/2003.
BI. REMIDA I. IBRAHIM kuanzia tarehe 30/9/2003.
BW. TITUS M. LYARUU kuanzia tarehe 8/9/2003.
BI. SEVERA SALVATORY kuanzia tarehe 1/9/2003.
BW. BANAGA M. KATABAZI kuanzia tarehe 8/10/2003.
BI. TRIPHONIA THADEI MNG'ONG'O kuanzia tarehe 15/9/2003.
BW. WILLIAM GEORGE MJEMA kuanzia tarehe 1/9/2003.

Kuwa Afisa Utumishi Daraja la III:–

BW. YUSUFU I. MSAWANGA kuanzia tarehe 2/8/2003.
BW. COSATO CHUMI kuanzia tarehe 18/9/2003.

KUBADILISHWA KAZI

Kuwa Afisa Utumishi Daraja la II:–

BIBI ROSE GEORGE MBEZI kuanzia tarehe 1/10/2003.
BW. MICHAEL GWISU MASANJA kuanzia tarehe 30/9/2003.

Kuwa Afisa Utumishi Daraja la II:–

BIBI MARIA F. KATEMANA kuanzia tarehe 8/10/2003.
BI. ANNA E. WIKETYE kuanzia tarehe 24/9/2003.
BW. JOSEPH M. KITUNDU kuanzia tarehe 1/9/2003.
BW. MATHIAS D. M. SIAME kuanzia tarehe 25/9/2003.
BW. BWAI B. MASHAURI kuanzia tarehe 10/9/2003.
BIBI SARAH B. MSALYA kuanzia tarehe 25/9/2003.
BW. EMMANUEL S. KUBOJA kuanzia tarehe 1/7/2003.

KUPANDISHWA CHEO

Kuwa Mwandishi Mwendesha Ofisi Kuanzia 1/7/2003

BIBI AGNES C. MBANZA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ELLA KIULA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI LILY S. E. MARUNDA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI DOTTO K. MLENDA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI LUIZA C. MKUMBUKWA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MOZA MALIMUSI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI LYDIA A. MWAIJANDE, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI OCTAVINA MALANGALILA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI HAFSA B. WALINGOZI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SOPHIA M. MVUMO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ALONGAMIKE KASUMUNI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI BISSURA H. MAGUO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI CLARA E. KIWANUKA, kuanzia tarehe 1/7/2003.

Kuwa Katibu Mahsusi daraja la I

BIBI BERNADETHA M. LUBOGO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. AUGUST KALORI LEKULE kuanzia tarehe 1/5/2003.

Kuwa Katibu Mahsusi daraja la II kuanzia 1/7/2003

BIBI ANNA E. MHINA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI JOSEPHINE KAJALE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SAFIA M. BAKARI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI RUKIA O. MAGOMA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI VERONICA CHIPATUKIRA kuanzia tarehe 1/7/2003.

Kuwa Mwandishi Mwendesha Ofisi daraja la I

BIBI CHRISTINA M. G. WENGA kuanzia tarehe 1/5/2003.

Kuwa Msaidizi wa Mtendaji Mkuu daraja la I Kuanzia 1/7/2003

BIBI LUIGIANA N. SANDU kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. AHMED A. HASSAN kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI THERESIA N. KITAMBI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. CORNEL J. UPUNDA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. MARY E. MWAMBOGELA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI JESTINA MSENGA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI BABRA MNDOLWA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ANNA GRACEWELL KILEWELA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MARGRETH B. FORODHA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ELIZABETH DOSLA GEAY kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. MARYAM A. PONDA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. ATIKI J. PANGAPANGA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SARAH NDOERA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI FELISTER KASHAIJA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. RHODA MNDEME kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MARTHA T. KANZAGA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. DIANA R. KYARA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI PILI M. MWAMBONA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. HERMAN J. T. MARCEL kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MODESTER B. S. PAUL kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI JACKSON E. MACHA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AUREA D. SHIRIMA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AGNES E. PANDISHA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. JEROME F. MHELELA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MERCY ELIZABETH ZUBERI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. ZABIBU S. NGATILA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. AHMED J. KWALO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. ERUSHA H. K. MASIJA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. MARY M. CHOMBO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. BLANDINA S. KIULA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. ALBERT H. MILANZI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. MICHAEL GILES MHINA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AMINA S. MTURUYA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. ODILIA WILLIAM kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ROSHAN R. FARAJI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MWANATE SAID kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI GRACE A. MBESWA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SHIJA S. KISONGO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI BETTY J. MOSHI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI NATALIA S. MASAMBA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI JUDITH R. MKOBA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. FRED R. C. HORE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. SILAS A. SABUNI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. ALPHONCE J. SHAYO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. WILLIAM F. SANGENI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AZIZA M. MWAMBO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. GEORGE A. KAUME kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MAIMUNA K. GOMINALI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. JAMES F. KILUVIA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI HAWA M. MFUTAKAMBA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI CHIKU J. SISYA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI FELICITAS K. KAYOMBO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI APRONIA RUTAIHWA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI JOYCE MWAIJELE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI IDRISA RAMADHANI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI LOUISA G. MWAMBE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI PRISCILLA V. MJALIWA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI PAULINA C. BAGOKA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI LEAH K. FEDUKA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MARY S. MAZENGO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI HALIMA H. MBILU kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI DELLY E. N. PONGOLANI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. ADOLF M. MCHEMWA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI BERNADETTA KASELLA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. HERMANA H. MAPUNDA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI EMILLIANA M. ADAM kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MARGARETH R. VAVA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI FLORENTINA K. MALOLA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI FATUMA S. S. MONDWE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI HAWA MLOWE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AGNES H. MZUKA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SHAN A. MAHMOUD kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. ISAACK A. MWASUBILA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI HADIJA R. LWENDO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI IDE RAPHAEL SANGA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. OMARI H. NGOLLA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. CECILIA A. MTUKA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. SOPHIA J. MABULA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI BASILISA M. MUNTHALI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. ALOYE P. MBISA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. HELENA A. AHELEKE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. ANYUMBATILE SAID SANGA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ZAINABU R. MKINZE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MWAHIYARI Z. YUSUFU kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MASUMBUKO E. MFANGA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI LUIBERT M. HATIBU kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MARY EDWARD SIAME kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI CLEMENTINA P. G. MMUNI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. ZAYUMBA A. R. ZAYUMBA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SALOME F. HAULE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ANGELINA M. MAYEYE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI LOICE G. M. MWITA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AGNES J. HILUKA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SANTIEL S. MBAJO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AGATHA MAKUMBULI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MWANAMTAMA H. MARANDU kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ANNA M. TARIMO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MWAJUMA A. BIRANGO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SUSANA D. OGUMA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI STEPHEN M. MKOKOTA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. MERCY L. MHOJA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. JULITHA S. MGOMBE, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ALICE E. NKWABI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SUSANA J. MDETE, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. HAWA E. CHOMBA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI LOUISA B. KAKOKERE, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. WINTAPA A. NTULU, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ADELAH L. RUGAIHURA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI CUNEGUNDA K. SAITOLOKI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. PHILEMON S. MTEWELLE, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ANGELINA MKUMBO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. ROSE ITALAZYO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI BERTHA G. MTALISI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. JOSEPH N. FREDERICK, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ELLA CHARLES RAJILA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI EMILIANA M. KITUNDU, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. DORAH J. MGONDAH, kuanzia tarehe 1/7/2003.

BIBI GERMANA D. CHIMWANDA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI FORTUNATA M. MWINGIRA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI DARIA MVULA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ELIZABETH MAJOGO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI RAHEL P. MBWAMBO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI CATHERINE D. I. KIJUU, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI THEREZA J. MAKWEA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI IPHIGENIA M. CHIWATA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI FADHILA S. MWINDADI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. FRANCIS X. A. NJOZI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI HAPPINESS A. KIHAMPA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. RAHAB W. MMBAGA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AGNES K. LUSINDE, kuanzia tarehe 1/7/2003.
Agnes O., Wandwi kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. MONICA K. KAPONGO, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. JEROME SHIBANI, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI GWANTWA J. K. LYAKURWA, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ANSILA C. SETEBE, kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI SUSANA B. MUSA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI AISHA S. KOMBO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI PULKERIA K. CHITIKITIRA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI JESCAR B. MWAKIPESILE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. MARTIN A. MTEGA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MARY J. MGAYA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MARY DARI SWEBE kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. EMILY H. AMLIMA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MATLIDA N. SETUMBI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. PAULINA OMBENI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI RAMADHANI H. ABEID kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI KIJOLI A. JONGO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI TATU S. MDINGI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI MWANTUM M. MTORO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI CATHERINE G. BUSUNGU kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. LAURENT EDWARD MLAY kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI EMERENTIANA M. SHIRIMA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI. LETICIA T. K. NTOKAMBALI kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. JOHN R. SHAFUNTO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI VICTORIA N. MUNUO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. WINFRIDA STEPHANO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI ZIADA A. WAIJAA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI HALIMA K. KASHUMBA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BIBI EXPERANSIA T. MAZIGO kuanzia tarehe 1/7/2003.
BI. CHRISTINA ROSE WAPALILA kuanzia tarehe 1/7/2003.
BW. HUMPHREY K. PYUZA kuanzia tarehe 1/7/2003.

Kuwa Msaidizi wa Mtendaji Mkuu daraja la II

BI. NIVONEIYA W. MGONJA.
BIBI AGATHA C. SWAI.

Kuwa Afisa Tawala Mwandamizi

BW. GEDION OSIAH A. MALABEJA kuanzia tarehe 1/5/2004.
BW. KARLO M. NACHIHANGU kuanzia tarehe 1/6/2004.
BIBI HAFSA S. DUDUMA kuanzia tarehe 1/6/2004.
BIBI AURELIA R. MATAGI kuanzia tarehe 1/6/2004.
BW. SHEUSHI J. MBURI kuanzia tarehe 1/6/2004.
BW. EDWARD J. NKEMBO kuanzia tarehe 1/6/2004.
BW. STEPHEN LEONE MUSHI kuanzia tarehe 1/6/2004.
BIBI JOAN JOSEPH MBUYA kuanzia tarehe 1/6/2004.

Kuwa Afisa Tawala daraja I kuanzia 1/5/2004

BIBI FLORA E. MSUYA kuanzia tarehe 1/5/2004.
BIBI GRACE J. SHESHUI kuanzia tarehe 1/5/2004.
BIBI ELIASIFU S. MLAY kuanzia tarehe 1/5/2004.
BW. XAVIER M. DAUDI kuanzia tarehe 1/5/2004.
BW. YONA S. MWAKILEMBE kuanzia tarehe 1/5/2004.
BW. OREST L. MUSHI kuanzia tarehe 1/5/2004.

KUTHIBITISHWA KAZINI

Ofisi ya Rais–Menejiment ya Utumishi wa Umma

Kuwa Afisa Tawala Daraja la III:–

BW. MICHAEL R. MAKOMBE kuanzia tarehe 17/4/2002
BW. RICKNEVILLE J. MWANRI kuanzia tarehe 26/7/2003
BIBI JULIANA KILASARA kuanzia tarehe 11/9/2002
BW. LUCIAS R. MWENDA kuanzia tarehe 6/8/2002

Kuwa Afisa Utumishi Daraja la III:–

BW. LAMECK S. MADYAGA kuanzia tarehe 1/7/1998